

ALIENTANGULIWA KATIKA SWALA.

Alietanguliwa katika swala ni yule ambae ilimpita rakaa au zaidi ya rakaa ndani ya swala, na akasimama kukamili zile ambazo zilimpita baada ya Imamu kutoa salamu ya pili ya kumaliza swala, atakuwa ni mwenye kuipata rakaa pale atakapo mdiriki Imamu kwenye rukuu, ama akiwa hatamdiriki Imamu kwenye rukuu basi itakuwa ameikosa rakaa pamoja na Imamu na itakuwa rakaa hiyo imempita.

Na inatakiwa kwa alietanguliwa anapoingia msikitini moja kwa moja akajiunge kwenye swala ya jamaa popote atakapo mkuta imamu ndani ya swala, sawa sawa amkute Imamu amesimama au amerukuu, amesujudu au popote pale yeye anatakiwa kuunga jamaa, haitakikani kusubiri mpaka Imamu aanze rakaa ya pili ndipo aunge sivyo, bali ataleta takbira ya kuhirimia swala kisha moja kwa moja ataunga swala pale alipomkuta Imamu isipokuwa kwa mwenye udhuru kama vile mgonjwa.

VYENYE KUBATILISHA SWALA.

1. Kuzungumza kwa makusudi hata kama maneno ni kidogo.
2. Kutoelekea qibla mwili wako wote.
3. Kutokea kitenguzi miongoni mwa vitengua udhu.
4. Kufanya harakati nyingi kwa kufuatana isipokuwa kwa dharura.
5. Kucheka ndani ya swala hata kama ni kidogo.
6. Atakapo zidisha rakaa, kusujudu, kisimamo au kikao kwa makusudi kufanya hivyo.
7. Kumtangulia Imamu kwa makusudi.